Kubadilisha hadi Masomo ya Mbali: Muhtasari wa Familia

Katika harakati za kupanga kurudi shuleni katika mwaka wa 2020-21, Shule za Umma za Jeffco zinaratibu upya Mpango wetu wa Masomo ya Mbali kulingana na yale tuliyojifunza kutoka msimu wa kuchipua wa 2020 wakati janga la COVID-19 lilipotokea. Muhtasari huu ulioratibiwa upya unaelezea jinsi shule zitakavyobadilisha na kutumia masomo ya mbali ili wanafunzi wetu waendelee na elimu yao iwapo mwongozo wa afya unaathiri masomo ya ana kwa ana.

MASHARTI YA KUBADILISHA NA KUTUMIA MASOMO YA MBALI

1) Iwapo Afya ya Umma ya Kaunti ya Jefferson (JCPH) itabainisha kuwa kaunti hiyo inapaswa kutekeleza tena amri ya afya ya umma ya Kukaa Nyumbani kutokana na ongezeko la visa vya maambukizi, Shule za Umma za Jeffco zitabadilisha na kutumia masomo ya mbali kwa wanafunzi wote.



2) Masharti yafuatayo yanaweza kusababisha kubadilisha na kutumia masomo ya mbali katika kiwango cha shule, daraja au kikundi.

Kisa cha Mtu Binafsi



Iwapo mwanafunzi au mfanyakazi atatambuliwa kuwa na maambukizi ya COVID-19, kikundi(vikundi) chake cha karibu kitawekwa katika karantini kwa siku 14 kuanzia siku ya kwanza ambayo mwanafunzi/mfanyakazi aliyeambukizwa alionyesha dalili za COVID-19.

Mkurupuko Mdogo

Iwapo kuna mkurupuko shuleni (mkurupuko unafafanuliwa kama visa viwili vya maambukizi ya COVID-19 katika vikundi viwili tofauti katika shule moja), shule hiyo itafungwa kwa wanafunzi wote kwa saa 24 kwa ajili ya usafishaji wa kina. Baada ya saa 24, wanafunzi wote watarudi kwa masomo ya ana kwa ana **isipokuwa** vikundi ambavyo vimeathiriwa moja kwa moja na visa vya maambukizi.

Mikurupuko Mingi



Iwapo kuna mikurupuko miwili katika siku 14, shule itabadilisha ifanye masomo ya mbali kwa siku 14 kuanzia siku ya kwanza ambapo mtu aliyeambukizwa hivi karibuni alipoonyesha dalili.

Mkurupuko Mkubwa

Iwapo kuna asilimia 5 au zaidi ya wanafunzi/wafanyakazi wasiohusiana walio na visa vilivyothibitishwa vya COVID-19 katika siku 14, shule itafungwa kwa siku 14 kuanzia siku ya kwanza ya dalili ambapo mtu wa hivi karibuni alipoonyesha dalili. Wakati huu, shule itabadilisha na kutumia masomo ya mbali.

KISA CHA MAAMBUKIZI YA COVID-19 NA HATUA ZINAZOFUATA

- Iwapo kuna kisa cha maambukizi ya COVID-19, Shule za Umma za Jeffco zitafanya kazi kwa kushirikiana na JCPH na kufuata Mchakato wa Karantini ulioundwa kwa ushirikiano. Mchakato wetu wa karantini unaambatana na mwongozo wa CDPHE wa visa na mikurupuko katika huduma za utunzaji wa watoto na shule.

- Wafanyakazi na wanafunzi wanaoonyesha dalili katika jengo watahitajika kwenda kwenye Chumba kilichotengwa cha Usalama cha Matibabu (sio chumba cha afya, kwani hiki lazima kiwe kimefunguliwa) hadi watakapokuwa salama kuondoka kwenye jengo hilo.

- RN wa Wilaya, Wasaidizi wa Afya, na wafanyakazi wengine walioteuliwa wana mafunzo ya kina kwa ajili ya Vyumba Salama vya Matibabu na udhibiti wa wanafunzi na wafanyakazi wanaoonyesha dalili. Ufuatiliaji kutoka kwa RN wa Wilaya utaendelea kwa wafanyakazi na wanafunzi wote walio na dalili ambao wameagizwa kwenda nyumbani.

- Uratibu wa pamoja na JCPH kuhusu visa vinavyoshukiwa na kuthibitishwa ni pamoja na:

    - JCPH itasaidia timu ya uongozi wa Shule za Umma za Jeffco katika kubainisha hatua za kuchukua kwa shule binafsi kulingana na kila kisa.

    - Barua za arifa zitatumwa na Mkurugenzi wa Huduma za Afya wa Shule ya Umma ya Jeffco na ushirikiano wa Idara ya Mawasiliano na usimamizi wa shule.

KUBADILISHA HADI MTINDO WA MASOMO YA MBALI

Siku ya kwanza baada ya tangazo la kubadilisha hadi mtindo wa masomo ya mbali

Shule binafsi zitabainisha kasi ya kuzoea masomo ya mbali (mara moja au baada ya kufunga kwa siku moja iwapo itachukuliwa kuwa muhimu na Uongozi wa Shule). Zitaamua ni lini wanafunzi watatarajiwa kutangamana mtandaoni. Wakati utaamuliwa ili kusaidia walimu kuanzisha mfumo wa masomo ya mtandaoni kwa darasa (madarasa) lao. Mikutano ya mtandaoni na usaidizi utapatikana kupitia timu ya Ed Tech. Shule zitatarajiwa kutuma ujumbe kwa familia zao mara moja na kuendelea kusaidia katika kuzoea mazingira mapya kunakoendelea kwa masomo ya mbali.

Miundo ya siku ya shule

Shule binafsi zitachapisha ratiba zao zinazoambatana na matarajio ya Wilaya. Ratiba zitasambazwa na shule wakati shule binafsi au Wilaya inapobadilisha na kutumia masomo ya mbali wakati wa mwaka wa shule.

ITIFAKI ZA MASOMO

Katika kuendeleza mafunzo kutoka msimu wa kuchipua, matarajio yamewekwa kwa shule kote Wilayani ili kutoa elimu ya hali ya juu iwe ni katika kuwahudumia wanafunzi kwa masomo ya mbali au ana kwa ana.

Mifumo ya Kawaida ya Usimamizi wa Masomo (LMS) itatumika katika Wilaya yote:

- Seesaw (PK-3)
- Google Classroom (3-12)
- Schoology (6-12)

Kila wiki, wanafunzi watatangamana na walimu wao katika mazingira ya ana kwa ana (Zoom au Google Meet).

Wanafunzi watapata angalau masaa 3 ya masomo ya moja kwa moja kila siku. **Masomo ya moja kwa moja** ni mbinu ambapo walimu na wanafunzi wapo mtandaoni kwa wakati mmoja kulingana na ratiba iliyowekwa. Mwalimu anatoa nyenzo za masomo na/au kazi katika wakati ulioratibiwa.

Masomo yasiyo ya moja kwa moja ni mbinu ambapo walimu na wanafunzi hawapo mtandaoni kwa wakati mmoja. Mwalimu anaweza kutoa nyenzo za masomo na/au kazi ambazo wanafunzi wanafaa kufanya peke yao, katika wakati wanaopendelea.

Sera za Utoaji Alama na Tathmini
Kwa sababu ya kughairiwa kwa tathmini ya jimbo wakati wa COVID-19, Jeffco itaendelea na kutumia miongozo ya sera za utoaji alama na mpango wa tathmini ili kubaini mahitaji ya wanafunzi wao. Wilaya itatoa MAP, Acadience, na Tathmini wa Utayari wa Chekechea (KEA) zinazoambatana na kalenda za utahini wa wanafunzi. Usaidizi wa familia utatolewa katika mitihani hii, ikiwa ni pamoja na yafuatayo:
Kipimo cha Maendeleo ya Kimasomo(MAP kwa daraja za 3-10) Usaidizi wa Familia kwa Tathmini za Mbali za MAP

- Kihispania
- Kichina
- Kivietinamu
- Kiarabu

Utathmini ya Acadience

Tathmini ya Mapema ya Chekechea (KEA) Usaidizi wa Familia (Chekechea)

Tafadhali wasiliana na shule yako kwa maelezo zaidi kuhusu sera mahususi za utoaji wa alama.

Mahudhurio
Mahudhurio ni muhimu kwa mafanikio ya mwanafunzi. Wasiliana na shule yako moja kwa moja ili upate maelezo zaidi kuhusu matarajio ya mahudhurio ya mbali. Mahudhurio ya mbali ya shule yanaweza kuhesabiwa kwa njia zifuatazo:

- Uwepo wakati wa mafundisho ya ana kwa ana;
- Kazi zilizokamilishwa nyumbani;
- Kuingia kwenye mfumo wa masomo ya mtandaoni;
- Kusaini fomu ya mtandaoni ili kuthibitisha kazi iliyokamilishwa nyumbani;
- Maonyesho ya mwanafunzi ya kujifunza;
- Kujibu barua pepe au mawasiliano ya mwalimu;
- Kutazama video za mafundisho zilizorekodiwa hapo awali; au
- Kuangalia au kushiriki kwenye majadiliano au vikao vya mtandaoni kupitia mifumo kama vile Zoom au Google Classroom.

Usaidizi wa Mwanafunzi
Usaidizi wa mwanafunzi kama vile utoaji wa elimu maalum na huduma husika, usawa, utofauti na ujumuishaji, masomo ya kijamii na kihisia, huduma za ushauri, kiingereza kama lugha ya pili na mengi zaidi utaendelea kutolewa katika mazingira ya masomo ya mbali.

MATAYARISHO YA MASOMO YA MBALI

Familia zinaweza kuwasaidia wanafunzi wajiandae kwa masomo ya mbali kwa kufanya yafuatayo:

- Wakati wanafunzi wapo katika masomo ya ana kwa ana, watahitaji kuzoea kwenda nyumbani kila usiku na Chromebook, iPad, kompyuta ya kupakata, chaja na vipokea sauti vya kichwani.

    - Iwapo mwanafunzi anahitaji kuomba kifaa, anapaswa kushirikiana na shule yake ili kubaini iwapo vifaa vya ziada vinapatikana.

- Wanafunzi watahitaji kuhakikisha wana muunganisho wa intaneti wa kasi ya juu nyumbani.
    - Kwa wanafunzi wasio na intaneti, mahali pa mtandao pepe panaweza kupatikana kwa malipo. Tafadhali wasiliana na shule yako.

- Jua majina ya mtumiaji na nywila za kuingia za mwanafunzi wako.
- Jisajili katika Nyenzo ya Kuweka Kubadilisha Nywila.
- Pata maelezo kuhusu jinsi ya kuwasiliana na shule yako kutoka nyumbani.
- Jua jinsi ya kuwasiliana na mwalimu kupitia Chromebook, kompyuta ya kupakata au iPad yako.
- Tayarisha eneo maalum ili kuweza kumakinika na masomo nyumbani.
- Kuwa na vitabu kadhaa vya kujisomea.
- Tumia rasilimali za teknolojia za kujisaidia mwenyewe ili kujibu maswali mengi ya kawaida kuhusiana na programu na teknolojia.
- Tazama Vidokezo vya Jeffco vya Masomo ya Mbali kwa Mwanafunzi.

USAIDIZI WA TEKNOLOJIA

Muunganisho wa Intaneti kwa Wanafunzi

Wanafunzi na familia zisizo na ufikiaji thabiti wa intaneti zinapaswa kuwasiliana na shule zao ili zipate usaidizi. Kisha wafanyakazi wa shule watashirikiana na wafanyakazi wakuu wa IT, washirika wa jamii (kama vile Wakfu wa Shule za Jeffco na Maktaba ya Umma ya Kaunti ya Jefferson), biashara, na wengine ili kuhakikisha wanafunzi wanapata intaneti ya nyumbani kwa masomo ya mbali. Pata chaguo za gharama nafuu za intaneti za kuzingatiwa.

Vifaa vya Wanafunzi

Wilaya ilitambua jumla ya vifaa ambavyo vinapatikana na imekuwa ikifanya kazi ili kuvisambaza tena ili kila mwanafunzi apate kifaa anachoweza kutumia kwa masomo ya mbali. Wanafunzi wote wa darasa la 5 na la 9 walipokea kifaa kipya mwanzoni mwa mwaka wa shule kama sehemu ya mpango wa TechForEd. Vifaa vinavyomilikiwa na shule walivyokuwa wakitumia vinasambazwa tena kwa viwango vya madarasa ya chini. Wanafunzi wetu wa darasa la 6 na la 10 walipokea vifaa kupitia mpango huu mwaka uliopita.

Usaidizi wa Wanafunzi na Familia Zao

Tunaendelea kuweka wafanyakazi wa huduma za simu ya usaidizi wa kitaalamu wa nje kupitia 303-982-3438 kwa wanafunzi na familia zao. Aidha, tumeunda chati ya mchakato ili kusaidia familia kujua watu wanaopaswa kuwasiliana nao kuhusu maswala ya kitaalamu. Tovuti yetu ya umma ina kurasa mbili nzuri za nyenzo: ukurasa wa usaidizi wa kifaa na ukurasa wetu wa nyenzo za kitaalamu, ambazo zinajumuisha nyenzo za Chromebook, iPad, Google Classroom, Schoology, SeeSaw na zaidi. Rasilimali nyingi za kitaalamu zilizounganishwa zimetafsiriwa katika lugha nyingi.

Vifaa vya Teknolojia

IT na Ed Tech zimeshirikiana ili kutoa na kutumia vifaa vya kidijitali na programu za ziada, kama vile Actively Learn,

Adobe Spark, Screencastify na Zoom, pamoja na kuboresha matumizi ya nyenzo za michakato iliyopo ili kuimarisha mazingira yanayobadilika ya elimu katika mwaka huu.
Familia zina idhini ya kufikia Programu ya Securly Home ili kufuatilia na kudhibiti shughuli za mwanafunzi wao kwenye vifaa vyao vya Jeffco. Wilaya pia ilinunua kifaa cha usimamizi wa darasa la Securly kinachotumiwa na walimu katika wilaya nzima. Mojawapo ya manufaa kuu ya kifaa cha Usimamizi wa Darasa la Securly ni kwamba inaweza kutumika kwa mazingira ya darasa la ana kwa ana na darasa la mtandaoni.

HUDUMA ZA VYAKULA NA LISHE BORA

Huduma za Vyakula na Lishe Borazitaendelea kutoa milo ya "kuchukua na kuondoka" kwa wanafunzi. Mahali na nyakati za huduma za milo ya "kuchukua na kuondoka" zitabainishwa na kuelezewa iwapo shule au wilaya itabadilisha na kutumia Masomo ya Mbali.

HUDUMA ZA UTUNZAJI WA WATOTO

Idadi ndogo ya maeneo na viti vya shule itapatikana kwa huduma za utunzaji wa watoto kwa wanafunzi wa darasa za PK-5 iwapo kutakuwa na kubadilisha na kutumia masomo ya mbali. Idadi ya maeneo na viti vinavyopatikana itabainishwa kulingana na sehemu ya miongozo ya afya ya umma wakati huo. Uamuzi kuhusu viti utafanywa kulingana na hitaji, kama vile wanafunzi ambao wanastahiki Vyakula vya Mchana Visivyolipishwa au Vilivyopunguzwa Bei (FRL).

MAWASILIANO NA FAMILIA

Shule za Umma za Jeffco zitaendelea kuwasiliana na familia wakati huu wa mpito na wakati wa masomo ya mbali. Wilaya itaendelea kutoa taarifa na maelezo muhimu kupitia jarida letu la barua pepe la *Taarifa kwa Jamii (Community Update)*. Shule na walimu watakuwa wakiwasiliana kuhusu ratiba zao mahususi, madarasa, na maelezo yanayohusiana na shule yao. Aidha, matangazo na taarifa muhimu zitasambazwa kupitia:

- Tovuti ya wilaya katika jeffcopublicschools.org
- Tovuti na vituo vya mitandao ya kijamii vya shule yako
- Majarida na barua pepe za wilaya na shule
- Upigaji simu na ujumbe wa maandishi
- Vituo vya mitandao ya kijamii vya wilaya:
    - Twitter
    - Instagram
    - Facebook
    - Twitter ya TeamJeffco
    - Instagram ya TeamJeffco
- Vyombo vya habari

Iwapo hupokei mawasiliano ya barua pepe, simu, au ujumbe, tafadhali angalia mipangilio ya maelezo yako ya mawasiliano katika Jeffco Connect au uwasiliane na ofisi ya shule yako kwa usaidizi zaidi.

Familia zote zinapaswa kupokea jarida la mtandaoni la Taarifa ya Jamii ya Wilaya. Iwapo hujajiandikisha au ulijiondoa hapo awali, jiandikishe ili ujiunge na orodha ya barua pepe za Taarifa za Jamii.

Usaidizi wa Wilaya wa Masomo ya Mbali	Nambari ya Simu
Simu Kuu ya Shule za Umma za Jeffco	303-982-6500
Ofisi ya Shule za Mkataba	303-982-6805
Miunganisho ya Jamii na Familia	303-982-1144
Usawa, Utofauti na Ujumuishaji	303-982-6559
Huduma za Vyakula na Lishe Bora	303-982-6748
Wenye Vipawa na Vipaji	303-982-6650
Huduma za Afya	303-982-7251
Shule ya Chekechea (Idara ya Masomo ya Chekechea)	303-982-1737
Safe2Tell	1-877-542-7233
Simu ya Usaidizi wa Jamii kuhusu Elimu Maalum	303-982-6682
Simu ya Dharura ya Usaidizi wa Kiufundi wa Familia	303-982-3438

restartjeffco.com